

Kamati ya ufundi ya serikali mtandao yakutana Dodoma

NA MWANDISHI WETU

KAMATI ya Ufundi ya Serikali Mtandao, imekutana kwa mara kwanza jijini Dodoma, kujadili mambo mbalimbali ikiwemo namna ya utekelezaji wa majukumu yake, kuhakikisha jitihada za serikali mtandao zinaimarika na kuleta tija kwa umma.

Kikao hicho kilifanyika jijini hapa, juzi katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kuongozwa na Kaimu Mwenyekiti Eric Kitali ambaye pia ni Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Akizungumza katika kikao hicho, Eric alisema kamati ipo kwa mujibu wa kifungu namba 17 cha sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kutoa ushauri wa kitaalamu, kuhakikisha utekelezaji wa serikali mtandao unakuwa ni wenye tija na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Mkurugenzi huyo alieleza kamati ina wajumbe wachache ikilinganishwa na idadi ya wizara na taasisi za serikali zilizopo, hivyo aliwasihaji wajumbe kutenda haki kwa kuwajibika na kuhakikisha wanatoa ushauri wenye tija eneo la TEHAMA kuhakikisha serikali mtandao inaimarika na kuleta tija kwa serikali.

"Ikiwa kamati hii itafanikiwa kuifanya mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma izungumze tutakuwa tumesaidia sana serikali, kwa kuwa itaokoa rasilimali fedha na rasilimali watu," alisisitiza.

Katibu wa kamati hiyo, Sylvani Shayo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Udhambi na Usalama wa TEHAMA e-GA, aliyataja baadhi ya majukumu ya kamati kwa mujibu wa kifungu Na 17 (4) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019 ni kupitia na kutoa mapendekezo kuhusu Sera ya Serikali Mtandao itakayotekelezwa katika taasisi za umma, kupitia na kutoa mapendekezo kuhusu mpango mkuu wa serikali mtandao na mkakati wake utakaotekelezwa na taasisi zote za umma.

Majukumu mengine ni kupitia na kutoa mapendekezo ya miradi na programu za kitaifa za serikali mtandao na kutoa miongozo ya kiufundi kutatua migogoro katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya TEHAMA kwa taasisi za umma.

Pia, kuishauri kamati ya kitaifa ya serikali mtandao kuhusu masuala ya serikali mtandao, kuandaa ripoti za robo mwaka na kuziwasilisha katika kamati hiyo na kutekeleza majukumu mbalimbali yatakayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Kamati ya kitaifa ya Serikali Mtandao.

Alisema kamati iliazimia kuweka mikakati ya kupunguza urudufu wa mifumo na kuhakikisha mifumo yote ya TEHAMA, katika taasisi za umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo Mkuu wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GoVESB).

Katika hatua nyingine, kamati ilimchagua Mkurugenzi wa TEHAMA Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Connie Francis, kuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Wajumbe wa kamati ni wakuu wa TEHAMA kutoka wizara na taasisi mbalimbali za serikali wakiongozwa na Mwenyekiti Priscus Kiwango kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Katibu Shayo